JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

HEADMASTER
KARATU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 62,
KARATU.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu kwa mawasiliano muhimu;**

**Mkuu wa Shule: +255787963136 / +255767963136**

**Makamu Mkuu wa Shule: +255767035317**

**Shule ya Sekondari KARATU**

**S.L.P 62 KARATU**

**Tarehe: ......................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**..................................................**
**S.L.P ........................................**
**..................................................**

Yah: **<u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KARATU HALMASHAURI YA KARATU MKOA ARUSHA MWAKA ..........</u>**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ......... na atasoma tahasusi ya .............
Shule ya Sekondari **KARATU** ipo umbali wa Kilometa **7** Magharibi mwa Mji wa **KARATU** Usafiri kutoka mjini **KARATU** unapatikana katika kituo cha mabasi **Karatu mjini.** Nauli ni Shilingi **3,000** kwa pikipiki na Shilingi **1000** kwa bajaji kwa mtu mmoja.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe ..../..../......... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..../..../......... na masomo yataanza tarehe ..../..../........

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

| S/N | AINA YANGUO |
|---|---|
| 1. | Suruali 2 nyeusi isiyobana na yenye urefu wa kutosha na upana wa miguuni usiopungua inchi 17 na rinda mbili yenye mkunjo chini (turn up), Koti nyeusi yenye vifungo vitatu na mpasuo mmoja nyuma (suti nyeusi) pamoja na Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali. |

| | |
|---|---|
| 2. | Shati 2 nyeupe mikono mirefu |
| 3. | Sweta nyeusi shingo V isiyo na alama yeyote. |
| 4. | Tai nyeusi |
| 5. | Suruali 1 kijani cha jeshi ya kushindia ( shamba dress) yenye urefu wa kutosha na upana wa miguuni usiopungua inchi 17 na rinda mbili yenye mkunjo chini (turn up) |
| 6. | Viatu vyeusi vya rangi, visiwe na visigino virefu vya kufunga na Kamba na soksi jozi mbili nyeusi. |
| 7. | Mashuka mawili light blue |
| 8. | Michezo: kwa wanafunzi wa sayansi jezi ya dark blue na wanafunzi wa Sanaa jezi nyekundu na viatu vya michezo kwa wote. |
| 9. | Truck suit ya light blue |
| 10. | Godoro ft 2½ kwa inchi 3 **iliyoshonewa (kitambaa) kava** ngumu. |
| 11. | Mto, Neti, foronya, blanketi na ndoo 2 yenye ujazo wa lita 10 kila moja na yenye mfuniko, brashi na kopo la kuogea. |
| 12. | Vyombo vya kulia chakula: Sahani, bakuli, kijiko na kikombe, pia unaweza kupata kwenye duka la shule kwa bei ya kawaida. |
| 13. | T.shirt yenye nembo ya shule inapatikana Duka la Shule - kwa Tsh15, 000/=. |
| 14. | Soksi nyeusi jozi nne (4) au zaidi. |

***NB: Nguo yoyote ya nyumbani hairuhusiwi shuleni.***

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:•

i. Madaftari ya canter book quire three yasiyopungua kumi (10) pamoja na graph pad 1.
ii. **Ream (A4)** (2).
iii. Vitabu; mwanao anatakiwa aje na vitabu vya masomo ya tahasusi aliyochaguliwa.
iv. Koti jeupe la maabara (lab-coat) linalovuka magotini kwa wanafunzi wa sayansi wanaoingia maabara.
v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wote wanaosoma masomo ya Sayansi, Hisabati, Geografia pamoja na uchumi.
vi. "Stop watch" na "dissection kit" kwa wanafunzi wa somo la bayolojia.
vii. Nguo za ndani za kutosha.
viii. Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo kulingana na Tahasusi yake;
- CBA: "Gumboots zake, Gadern hoe 1, forked hoe 1, watering can 1, jembe 1"
- CBG: Jembe 1, mkasi wa kukatia maua (fance) 1, na sabuni ya maji lita 5.
- EGM: Jembe 1, panga 1, chelewa 1 na sabuni lita 5.
- HGE: Hardbroom 1, jembe 1, dawa ya chooni lita 5 na sabuni lita 5..
- HGK: Mopa 1, soft brush 1, sabuni ya maji lita 5 na dawa ya chooni lita 5.
- HGL: Mopa 1, soft brush 1, sabuni ya maji lita 5 na dawa ya chooni lita 5.
- HKL: Jembe 1, panga 1, sabuni ya maji lita 5 na dawa ya chooni lita 5.
- PCB: Kwanja 1, reki 1, jembe 1 na sabuni lita 5.
- PCM: Beleshi 1, reki 1, kwanja 1 na sabuni lita 5.
- PGM: Jembe 1, reki 1, kwanja 1 na sabuni lita 5.

## 2.3 Michango mbalimbali

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi | Akaunti |
|---|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule. | 65,000/= | 40910001047 (KARATU SEC EK NMB) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Tahadhari kwa mwaka | 5,000/= | |
| 4. | Nembo kwa mwaka | 5,000/= | **Aje nazo mkononi** |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= | |
| | **Jumla** | **80,000/=** | |

**Mwanafunzi aje na pay bank slip (PBS) wakati wa kuripoti ikiwa imeandikwa jina kamili la mwanafunzi kama mlipaji.**

**NB**: Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na **Bima ya Afya na kwa wasio na Bima wanatakiwa kuja na shilingi 50,400/= kwa mwaka** iii **kumwezesha kupata Bima ya NHIF,** hii ni kutokana na changamoto za kimatibabu tunazozipata.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele au kufuga nywele.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Cheti cha kuzaliwa, cheti cha matokeo ya kidato cha nne (result slip)
iii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iv. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA S**

**ni ya ... hule ..**

**la Ml ... le: HU ... FA**

2:z''@jii:E|Win
zrj$a,@i»

Mhuri wa Mkuu wa Shule ………….,………f-•——-rlJ,

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule: +255787963136 / +255767963136
- Makamu Mkuu wa Shule: +255767035317
- Mwandamizi Taaluma: +255753008761
- Mwandamizi Malezi: +255753114972

Kumb.Na.KSS/K.4/Vol.3/84

**KUPIMAAFYA**

Mwanafunzi………………………………………Andika ndiyo katika nafasi mbele ya ugonjwa ambao ulikwishaugua au unaugua:

1. Kifua kikuu ……………………
2. Ugonjwa wa mayo……………………
3. Ugojwa wa figo……………………
4. Ugonjwa wa akili……………………
5. Ajali kubwa……………………
6. Pumu……………
7. Vidonda vya tumbo……………………
8. Kifafa ……………………
9. Upasuaji mkubwa……………
10. Ulemavu

**KIOFISI TU**

……………………………………………………

……………………………………………………

**KWA MATUMIZI YA MGANGA MKUU WILAYA/MKOA**

Tafadhali mpime mtajwa kama afya yake inamruhusu aendelee na masomo ya Sekondari kidato cha **TANO.**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

Pamoja na haya zingatia maelezo ya mwanafunzi hapo juu.

**MAELEZO YA MGANGA**

……………………………………………

……………………………

……………………………

…………………

**JINA LA MGANGA**

**CHEO** ……………………………………

**TAREHE**

**SAINI** ..

**MUHURI**

Kumb: Na.KSS/K4/V0L.3 /84

**TAARIFA JUU YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

1. Mzazi wa ....................................................................................................................Tahasusi ya ......................
2. Jina kamilila mzazi/mlezi...........so<<.do.d..os.
3. Umri.........S.O..
44. Kazi.........0SO.S0O.SO.O0...
5. Anuani ya nyumbani .................,
6. Namba ya simu za Mzazi/Mlezi............................
7. Kijiji.............................Kata........................Tarafa.....................Wilaya.............................. Mji............... Mkoa...............................
8. Uraia............S.O
9. (a)Dini ya mzazijmlezi..............................
10. Dhehebu unalotaka mwanao alelewe............. ..ass...........................

11. Anwani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo ...............................................

12. Anwani ya kazini ikiwa inatofautiana na hiyo hapo juu kila inapobadilika utuarifu rasmi kwa barua kupitia kwa mkuu wa kituo au mwenyekiti wa kijiji chako.

13. Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni sahihi na kweli

Jina la mzazi/mlezi.............ssssO.Sss0sOSsssss0oss.a

Saini.......ss«sos·s0.

Tarahe..........sos.•

Ninaahidi wakati wote kushirikiana na kusaidiana na walimu katika kumlea kijana wangu awe na tabia nzuri siku zote, awe mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Nitatimiza mahitaji yake yote kulingana na miongozo ya shule. Juu ya hayo naelewa kuwa mwanangu akienda kinyume na sheria za shule hatua za kinidhamu zitafuata ikiwemo kufukuzwa shule.

**Jina la Mzazi/Mlezi**........................................................

**Saini**.......,,,,,,,,,,,..,,,,,,,,,,,..


**Tarehe**.....,,,,,,,,,..,,,,,,,,,,,..

# Rangi za sare za shule

Rangi ya suruali ya shule (nyeusi)



Rangi ya kitambaa cha suruali ya kushindia (kijani cha jeshi)



"Track suit" kwa ajili ya kushindia



## Vitabu anavyotakiwa kuwanavyo mwanafunzi;

**Kwa wanaosoma soma la historia;**

(a) History for advanced secondary schools students Book form five by Tanzania instuite of education 2024.
(b) Essential in advanced level history paper I by SALEH YASSIN
(c) Essential in advanced level history paper II by SALEH YASSIN
(d) Learning advanced African history Book one and two by IDRISSA RAMADHANI MSUYA.

**Kwa wanaosoma soma la Kiswahili;**

(a) HGK-Vuta n' kuvute, usiku utakapokwisha, chungu tamu.
(b) HKL- Mfadhili, fungate ya uhuru, kimbunga.

**Kwa wanaosoma soma la jiografia;**

(a) Physical geography for advanced secondary schools students book (form five and six)
(b) Practical geography for advanced secondary schools students book (form five and six)

Kwa wanaosoma soma la uchumi;

(a) Basic economics Tayebwa B&Mugisha B. fifth edition.
(b) Basic economics Tayebwa B&Mugisha B. question&answers.

**Kwa wanaosoma soma la kingereza;**

(a) Advanced level English oxford
(b) A practical approach 2" edition by Nicholaus Ashel.

**Kwa wanaosoma soma la fizikia;**

(a) Nelkon & Parker (1995) advanced level physics 7" edition. Longman international education.
(b) Chand S. 2008 principal of physics for class 11 and 12 Newdell.

**Kwa wanaosoma soma la biolojia;**

(a) Yaylor, D. J. (1997) Biological Science, Cambridge University Press
(b) Susan Toole - Understanding Biology.
(c) Msaki, L (2003) Cell Structure.
(d) Msaki, L(2003) Systematics and Classification.

**Kwa wanaosoma soma la kemia;**

(a) Conceptual Chemistry - Chand S.K.
(b) Chemistry in Action - Michacl Freematle
(c) Physical chemistry for A-Level and Undergraduate:
(d) Mkayuba and Ddungu.
(e) Advanced Inorganic Chemistry Part I and I] - TIE.
(f) Soil and Environmental Chemistry.

**Kwa wanaosoma soma la hisabati;**

(a) Backhouse, Pure Mathematics I
(b) Backhouse, Pure Mathematics 2
(c) Shayo Leonard, Advanced Mathematics Vol. I.

**Kwa wanaosoma soma la kilimo;**

(a) Agriculture for advanced secondary school students book form five TIE

**Vitabu vingine ni pamoja na vya masomo ya;**

1. Historia ya Tanzania na maadili;
2. Academic communication